

## **BALOZI BARAKA LUVANDA AJUMUIKA PAMOJA NA TIMU YA WAOGEEAJI YA TANZANIA KATIKA MASHINDANO YA DUNIA YA MICHEZO YA KWENYE MAJI FUKUOKA 2023**

Tarehe 23 Julai 2023 Balozi Baraka Luvanda alijumuika pamoja na Timu ya waogeeaji ya Tanzania iliyoshiriki katika Mashindano ya Dunia ya Michezo ya kwenye Maji ya Fukuoka 2023 ( World Aquatics Championship Fukuoka 2023) iliyofanyika kuanzia tarehe 19 hadi 31 Julai 2023. Timu hiyo ilijumuisha wachezaji wanne ambao ni: Bw. Hilal Hemed Hilal, Bw. Collins Phillip Saliboko, Bi. Sophia Anisa Latiff na Bi. Ria Ninad Save ambao walishiriki mchezo wa kuogelea. Aidha, timu hiyo ilisindikizwa na Bi. Inviolata Itatiro, Katibu Mkuu wa Chama cha Waogeeaji Tanzania (TSA), Bw. Alexander Mwaipasi, Kocha wa Timu, na Bi. Asma Hemed Hilal, Mjumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Nidhamu ya Michezo ya kuogelea ya dunia.

Balozi Luvanda alijumuika na timu hiyo katika ufunguzi wa mchezo wa kuogelea na kupata fursa ya kuzungumza nao masuala mbalimbali kwa ajili ya kuwatia moyo na kuwatakiya kila la kheri katika mashindano ikiwa ni pamoja na kuwataka waendeleo kuongeza bidii katika mchezo huo.

Kwa upande wake, Bi. Inviolata alimshukuru Balozi Luvanda kwa niaba ya timu nzima kwa namna alivyoweza kujumuika na timu hiyo mjini Fukuoka na kuwatia moyo wachezaji, jambo ambalo limewafurahisha na kuwatia chachu ya kufanya vizuri zaidi. Aliongeza kuwa mchezo wa kuogelea unaendelea kukua nchini Tanzania na endapo Serikali itautilia mkazo na kuupa kipaumbele kama michezo mingine unaweza kutoa mchango mkubwa kwa kutoa wachezaji wakubwa watakaoweza kushindana kimataifa.

Vilevile, alisema kutokuwepo na uwanja wa kimataifa wa mchezo huo unaleta changamoto kwa wachezaji kufanya mazoezi nchini Tanzania na hivyo kuwalazimu kwenda kujifunza na kufanya mazoezi nje ya nchi. Hivyo ametoa wito kwa Serikali kufikiria suala la kujenga miundombinu wezeshi kwa mchezo huo ikiwa ni pamoja na kujenga uwanja wa kimataifa utakaowezesha wachezaji wetu kujifunza ndani ya nchi lakini pia kwa nchi kuweza kuwa mwenyeji wa mashindano ya kimataifa.

Mashindano haya ni sehemu ya maandalizi ya michezo ya Olimpiki inayotarajiwa kufanyika mwaka 2024 mjini Paris, Ufaransa.